KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 19, Issue 1

11th Rabiul Awwal 1433

3rd Feb, 2012

HAKI ZA JIRANI YAKO [PRT 2]

KULINGANA NA SUNNAH NA MFANO WA SALAF

Na: Sheikh Ali Hasan ibn Abdulhameed al-Halabi

MAKEMEO KUHUSIANA NA BAADHI YA RIWAYA ZILIZONASIBISHWA KWA MTUME (صلى الله عليه وسلم) KATIKA SOMO LA UJIRANI

1. JIRANI KABLA YA NYUMBA:

Hii imepokewa naat-Twabaraani katika al-Mu'jam al-Kabeer (4379), Abu'l-Shaykh katika al-Amthal (232), al-Khatib katika al-Jami'li Akhlaq ar-Rawi wa Adab as-Sami' (3/291) na al-Quda'i katika Masnad ash-Shihaab (709), kwa kupitia kwa Aban ibn al-Muhabbar kutoka kwa Sa'id ibn Ma'ruf ibn Raafi' ibn Khadij, kutoka kwa babake, kutoka kwa babu yake, kwa maneno:

"Tafuta Jirani kabla hujatafuta nyumba."

Amesema as-Sakhawi, katika **al-Maqaasid al-Hasanah** (No. 163): "Ibn al -Muhammar ni Matruk [yaani; Hadeeth zake hazikubaliwi]; Yeye pamoa3ja na Sa'id hawawezi kutegemewa katika kuthibitisha chochote."

Imaam adh-Dhahabi amepokea hadeeth (Mizan al-'l'tidal 15/1) kutoka kwenye riwaya Munkar (ngeni) za ibn al-Muhabbar!

2. MAJIRANI NI SAMPULI TATU:

Al-Bazzar (Musnad, 186-*Zawa'idah*) amesema: Abdullaah ibn Muhammad Abu'l-Rabi' al-Haarithi amepokea (*haddathana*) yakwamba Muhammad ibn Isma'il ibn Abi Fudayk amepokea: Abdur-Rahman ibn al-Fudhayl ametupasha (*akhbarana*) kutoka kwa (*'an*) Ata al-Khurasani kutoka kwa al-Hasan kutoka kwa Jaabir ibn Abdullaah aliyesema: "Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): 'Majirani ni sampuli tatu: Jirani aliye na haki moja, ambayo ndiyo idadi ya mwisho miongoni mwa haki za ujirani; Jirani aliye na haki mbili; na Jirani aliye na haki tatu. Ama kuhusu jirani aliye na haki moja, si mwengine ila ni Jirani mshirikina (ambaye hana uhusiano na wewe), aliye na haki ya Ujirani. Ama kuhusu Jirani aliye na haki mbili, si mwengine ila ni Muislamu aliye na haki ya Uislamu na haki ya Ujirani. Ama kuhusu Jirani aliye na haki tatu; si mwengine ila ni Jirani Muislamu anayehusiana na wewe; huyo ana haki ya Uislamu, haki ya Ujirani na haki ya uhusiano wa kizazi.'"

Amesema al-Bazzar: "Sisi twaijua hadeeth hii kwa kupitia kwenye isnad hii peke yake."

Amesema al-Haythami (*Majma' az-Zawaa'id, 8/164*): "Sheikh al-Bazzar 'Abdullaah ibn Muhammad al-Harithi ni mrongo [yaani; Mzushi]."

Vilevile hadeeth hii imepokewa na Abu'l-Shaykh, ad-Daylami na at-Twabaraani (*ath-Thowab na Sharh al-Ihyaa', 6/304*), na al-Hasan ibn Sufyan (Musnad), aliyesema [angalia pia katika al-Isbahani, Takhrij al-Ihyaa' (1837-chapa ya Saudi); na at-Targheeb wa'l-Tahrib (843)]: "al-Husayn ibn 'Issa al-Bustani amepokea yakwamba Muhammad ibn Abi Fudayk amepokea kutoka kwa Abdur-Rahman ibn Fudhayl."

Pia imepokewa na Abu Nu'aym, katika Hilyah al-awliyaa' (5/207) kutoka kwa Abu 'Amr ibn Hamdan kutoka kwa al-Hasan ibn Sufyan. Hii ni riwaya itokayo kwa mzushi al-Harithi."

Hadeeth hii ni dha'if kwa sababu ndani yake muna kasoro mbili (*'illatan*).

1. Udhaifu (*Dha'f*) wa Ataa' al-Khurasani. Kuliwahi kuwepo na baadhi ya midahalo kuhusiana na udhaifu wa Ataa' katika hadeeth hii. Ameipokea ibn 'Adiyy katika al-Kaamil (5/1818) kwa kupitia kwa Suwayd ibn Abdul'Aziz– ambaye ni dhaifu-kutoka kwake kutoka kwa 'Amr ibn Shu'ayb kutoka kwa babake kutoka kwa babu yake.

2. Al-Hasan hakuisikiya kutoka kwa Jaabir; angali kwenye Jami' al-Tahsil (Uk.163) cha al-'Ala'i.

3. **Mtume (صلى الله عليه وسلم) amewasisitiza watu kuchunga haki za Majirani zao hata wakawa mbali kwa kiasi cha nyumba saba."**

Riwaya hii haina msingi wowote. Ingawaje ni mas'ala yaliyo kwenye Sunnah kwa ujumla, juu ya kwamba kuchunga haki za majirani ni miongoni mwa Sunnah zilizothibitishwa, makisio ya uchungaji huo wa haki kwa kiasi cha umbali wa nyumba saba hayana msingi katika riwaya yoyote yenye kunasibishwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم). Na Allaah ndiye Mjuzi zaidi.

MTU NA AMUHUDUMIKIE VIPI JIRANI YAKE IKIWA YEYE SI MUISLAMU MTEKELEZAJI WA KI-SUNNI?

Iwapo jirani yako ni Muislamu-Mtekelezaji wa dhehebu la Sunni, basi hapana budi umuwajibikie haki zote zilizotangulia katika makala haya..

Lakini ikiwa jirani yako atakuwa na hatia ya Madhambi Makubwa, basi hafai kuwachwa peke yake. Ikiwa anatenda madhambi kwa siri, nyuma ya milango iliyoshindikwa, basi mpuuze na ufumbe macho yako juu ya ayafanyayo, lakini ikiwa waweza kumnasihi kwa njia ya siri, basi hilo ni bora kulitenda.

Na lau kama anafanya hayo kwa dhahiri na kujifakhiri, kwa mfano mtoza ushuru au mla-riba, basi wachana nae huyo.

Lau kama ana kawaida ya kuzikosa swala kwa wingi, basi endelea kumkumbusha juu ya mambo mazuri (*al-Ma'ruf*), na umkatishe tamaa katika kutenda kwake maovu (*al-Munkar*), au kama si hivyo basi muepuke kwa ajili ya Allaah-pengine hili huenda likawa

YALIYOMO

HAKI ZA JIRANI YAKO 1 - 4

TANGAZO LA DARSA- MAZRUI 4

na athari itakayomfaidisha yeye. Lakini usiwache kumuamkua, kuzungumza nae, na kumpa zawadi.

Lau kama ataendelea kuwa mkaidi na uovu wake, basi muepuke kabisa, na ujaribu kuhama kwenye mazingira mengine ya ujirani, kwa sababu kama ilivyotangulia kutajwa hapo awali, yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliomba hifadha kwa Allaah na Majirani waovu kwenye nyumba ya mtu ya kudumu.

Iwapo Jirani yako ana tabia ya kutojali kwa wanawake na wala hana hisiya za wivu kuhusiana na heshima ya wanawake wa nyumbani kwake, au wanawake wa nyumbani kwake hawako katika njia iliyo nyoka, basi mueouka na ujitahidi kuwakinga wasimsumbue mkeo, kwani hayo huwenda yakachangia kwenye uovu mwingi.

Uwoga, vilevile, udhaifi wa nafsi yako mwenyewe: usiingie kwenye nyumba hii, na ukate njia zote za mawasiliano na yeye ...

... Lau kama utadharau kusikiza ushauri huu, basi huwenda matamaniwa ya moyo wako yakakuzidi, na hutoweza kujiongoza nafsi yako, mwanayo, mfanyi kazi wako au dadako [yaani; mafungamano yote baina ya jamii yako na jamii ya jirani wabaya wasiojali yakatiliwe mbali]. Kama waweza kuwashawishi watu kama hao wahame kutoka katika mazingira ya jiranini mwako, basi hili na litekelezwe, kwa upole, na utaratibu, lakini kwa msimamo thabiti.

Lau kama jirani yako ni Raafidhi, au anahusika kwenye mambo ya Uzushi katika Dini (*Bid'ah Kabirah*), na ukawa wewe umeamua kumfundisha na kumuongoza, basi jaribu kadiri ya uwezo wako. Kama huwezi kufanya hivyo, basi jiepushe nae mbali, na wala usijaribu kujenga urafiki wowote au uhusiano nae; ni bora hata kuhama mahali hapo kabisa.

Lau kama katika ujirani wako-nyumbani, kwenye soko au shambani-ni Myahudi au Mnaswara, basi mtendee wema na usimsumbue. Ama kuhusiana na wale wenye kujishughulisha mno na kukubali ualishi wa [Mayahudi na Manaswara] Majirani, wenye kujenga urafiki nao na kujikurubisha na wao sana, basi Allaah (سبحانه وتعالى) amesema (tafsiri ya maneno yasemayo): **"Huwapati (huwaoni) watu wanaomuamini Allaah na siku ya mwisho, kuwa wanawapenda wale wanaompinga Allaah na Mtume wake; hata wakiwa ni baba zao au watoto wao au ndugu zao au jamaa zao. Hao ndio ambao (Allaah) ameandika (amethibitisha kweli kweli) nyoyoni mwao imani na akawatia nguvu kwa roho itokayo Kwake ...** [al-Mujaadalah 58:22]

Ikiwa [Mnaswara au Myahudi] huyu jirani yako pia anahusiana na wewe, basi hapana shaka yakwamba haki zake na ziheshimiwe. Lau kama mmojawapo wa wazazi wako ni Myahudi au Mnaswara, basi haki za wazazi na jamii zitakuwa ni juu ya haki za Majirani, kwahiyo, heshimu haki mbalimbali zenye kuwastahiki watu. Usianzishe maamkuzi (*Assalaamu 'alaykum*) kwa Majirani wa Ki-Yahudi au Ki-Naswara; iwapo wao watakuamkua, kwa hiyo wajibu kwa ufupi (*wa'alaykumussalaam*). Inaruhusiwa kubadilishana maamkuzi kwa mukhtasar baada ya kujulia hali zao (hujambo?) lakini usizidishe maamkuzi kama hayo, kama alivyosema Allaah (سبحانه وتعالى) (tafsiri ya maneno yasemayo): **"... Basi hivi karibuni Allaah ataleta watu ambao atawapenda, nao watampenda, wanyenyekevu kwa Waislamu (wenzao), wenye nguvu juu ya makafiri (al-Kaafirin)**[al-Maa'idah 5:54] Mu'min anatakiwa kuwa ni mkarimu kwa mu'min mwenzake, na anatakiwa ajizuiye kiasi fulani na wasio-Waislamu, kama ishara ya fakhri ya Uislamu. Haliyakuwa hatufai kuwasumbua, tusiamiliane nao kama tunavyo amiliana na Waislamu wenzetu.

HITIMISHO:

Hizi ndizo haki za Majirani, zinazowajibika bila ya kujali iwapo jirani yako ni Muislamu au Kafiri, Muislamu Sunni au Mzushi, Mswalihina au Muislamu-jina ... Haki za ajabu na zenye kushangaza, zinazotumika ulimwengu mzima zinaweza kuleta furaha katika ulimwengu huu na pia ulimwengu ujao. Kwa hiyo tunajua yakwamba umasikini unaoangamiza wana-adamu katika kila pembe ya Ulimwengu umeletwa kutokana na ukosefu wa Waislamu wa kweli katika nafasi za mamlaka na uwezo, na kwa sababu misingi ya Uislamu ya uadilifu imepotezwa nyuma ya mifumo isiyokuwa na maendeleo, iliyotengenezwa na watu, ambayo haikuwaletea wana-adamu isipokuwa ubakhili, umasikini, unyonyaji, njaa na aibu ... katika zama za usafiri wa angani, makombora, satelite na kutuwa juu ya mwezi!

Shirika la Ulimwengu la Ukulima na Vyakula [The World Agriculture and Food Organisation], lililofungamana na Umoja wa Mataifa [UN] lilitangaza katika mwaka wa 1975 yakwamba baina ya Milioni 20-100, watu katika bara la Afrika na Asia watakufa katika miaka ijayo. Lau kama hali hii itaendelea, basi watu Milioni tatu watakufa kwa njaa kila wiki. Baina ya watu Milioni 460-1,000 walikuwa tayari washaathirika kutokana na utapiamlo.

Katika wakati ambapo njaa inaponyemelea kwenye bara la Asia na Afrika, tunaona yakwamba katika sehemu nyengine za Ulimwengu, Magharibi (Ulimwengu wa Demokrasia!)- ulimwengu tajiri wenye kujumuisha 20% ya idadi ya watu ulimwenguni, lakini inapeleka 80% ya utajiri wa ulimwengu– wanafanya juhudi kubwa katika kuuzuiya utajiri huo. ...

Kwa hiyo, katika mwaka wa 1975, Brazil waliteketeza maelfu ya tani ya Kahawa, kwa ajili ya kuihifadhi bei yake katika soko la ulimwengu. Iliwagharimu Soko la Ushirika la Ulaya $50 Millioni kutaifisha na kuharibu vyakula na mbegu za Ukulima zilizokuwa ni uzalishaji wa ziyada kwenye mahitaji yao wenyewe, kwa ajili ya kuzihifadhi bei zao juu. Amerika hulipa Dola Millioni elfu moja kila mwaka katika kuwafidia wakulima kwa kutozalisha aina fulani za mimea, kuzilinda bei zao. Wakulima wa ki-Amerika huuwa na kuwazika ma-kumi ya ma-elfu ya Ndama, ili wazihifadhi bei za nyama ... katika wakati ambao, kwenye mwaka huo huo, ma-kumi ya ma-elfu ya watu walikufa kutokana na njaa katika Bara la Afrika, Asia na Amerika ya Kusini!

Hiyo ndiyo tafauti kubwa iliyoko baina ya Ustaarabu wa Uislamu wa ki-ubinadamu, usomruhusu mtu hata kumkera na kumsumbua Jirani yake kutokana na harufu nzuri ya mapishi yake yenye kutamanisha, na Ustaarabu wa Ki-Magharibi wa kutamani vitu, wenye kuwatisha ma-Millioni kwa njaa na vifo. Ni kudhalilishwa kulioje kwa wenye kuyakimbilia mifumo ya vitu, ema ya ki-Mashariki au ki-Magharibi, katika giza tupu la Jaahiliyyah! Na ni ukubwa wa kiasi gani wa majukumu ya Waislamu kuubeba mwangaza wa Taa (*Nur*); "kutokamana na mti uliobarikiwa ... Si wa kutoka Mashariki wala si wa ki-Magharibi!

Ni kwa Uislamu Peke yake ndipo udhaifu wa ki-Jaahiliyyah, utakapofichuliwa, na kwa Muangaza wake tu ndipo zitakapo angaziwa nyoyo na fahamu, na wana-adamu watakaporegeshwa kwenye uongofu wa sawa, usalama na kufuzu.

Sasa Jee, patakuwa na yoyote mwenye kuwaidhika?

MWANAMKE HANAJISIKI KWA AJILI YA HEIDH AU KUTOKWA NA DAMU YA MAZAZI

SUALI: Mke wangu amejifungua (amezaa) na mmojawapo wa marafiki zangu akanizuiya nisiingie hapo nyumbani kwangu, kwa madai yakwamba ati hairuhusiwi kwa mtu kula chakula chochote kilichotayarishwa na mwanamke atokwae na damu ya mazazi. Huzingatiwa hali ya mwanamke huyu kuwa amenajisika kimwili na kimaumbile. Natumai utanisaidia katika mas'ala haya. Kulingana na nijuavyo mimi, wanawake wenye kutokwa na damu ya mazazi hawaruhusiwi kuswali, kufunga au kusoma Qur'aan?

JAWABU: Mwanamke hanajisiki kwa ajili ya heidh wala kutokwa na damu ya mazazi. Hakatazwi mtu kula nae wala kugusana nae kimwili, maadamu sehemu yake ya tupu itaepukwa. Hatahivyo, ni makuruhu kugusana na sehemu za baina ya kitovu na magoti peke yake. Hii ime-egemezwa juu ya aliyoyapokea Muslim kutoka kwa Anas (رضي الله عنـــه): Miongoni mwa Mayahudi, pindi mwanamke akiwa katika heidh, huwa hawali chakula na yeye. Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلّم): "Fanyeni nao kila kitu (mupendavyo, kama kawaida yenu), isipokuwa musijamiiane nao."

Al-Bukhaari na Muslim pia walinukuu kutoka kwa 'AA'ishah (رضي الله عنهما) aliyesema yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلّم) alikuwa akimwambia ajifunge kitambara cha kiuno na kisha alikuwa akiamiliana nae kimwili haliyakuwa yuko katika heidh. Hakuna athari yoyote juu ya kula nae au kula chakula alichokitayarisha, kutokamana na kuharamishwa kwa swala, kufunga na kusoma Qur'aan akiwa kwenye heidh na kupata damu ya mazazi.

Kamati ya Wanavyuoni.

KUTUMIA TEMBE ZENYE KUZUIYA HEIDH:

SUALI: Kuna tembe zenye kuzuiya heidh au kuicheleweshe kutokea. Jee, mwanamke anaruhusiwa kutumia tembe kama hizo katika wakati wa Hijjah kwa kuchelea heidh yake isimjie?

JAWABU: Na'am, inaruhusiwa kwa mwanamke kutumia tembe zenye kuzuiya heidh katika wakati wa Hijjah kwa kuichelea heidh yake isimjie. Lakini jambo hilo ni baada ya kumtaka shauri Daktari atakae kumuhakikishia yakwamba afya yake haitoathirika. Vilevile, anaweza kufanya kama hivyo katika mwezi wa Ramadhaan ikiwa atapendelea kufunga na watu.

Kamati ya Wanavyuoni

KUKATIKA KWA DAMU KATIKA WAKATI WA HEIDH:

SUALI: Mara nyengine hunitokea, katika wakati wa heidh yangu, yakwamba hupata damu kwa siku nne kisha mara husimama kutoka kwa siku tatu. Kisha katika siku ya saba, damu hunirudia, lakini haiwi ya nguvu kama ile iliyotangulia. Kisha hugeuka na kuwa rangi ya hudhurungi au kahawia (Brown) mpaka katika siku ya kumi na mbili. Natumai utanioongoza juu ya jambo la sawa katika suala hili.

JAWABU: Masiku ulioyoyataja, siku ya nne na siku ya sita, ni masiku ya heidh. Hufai kuswali wala kufunga katika masiku hayo. Haifai kwa mumeo kukuingilia katika siku hizo. Itakupasa ujitwahirishe (utekeleze Ghusl) baada ya siku nne kisha uswali na mumeo ataruhusiwa kuingiliana na wewe wakati huo baina ya siku nne na siku sita. Pia hakuna uharamu juu ya kufunga kwako. Ikiwa hayo yatatokea katika mwezi wa Ramadhaan, utawajibika kufunga. Na utakapotwahirika baada ya hizo siku sita, itakulazimu utekeleze Ghusl, uswali na ufunge kama ilivyo katika wakati wowote za kutwahirika. Hii ni kwa sababu ada ya kila mwezi inaweza kuongezeka na kupungua. Mara nyengine masiku yake hushikana pamoja na mara nyengine huwa mbalimbali. Twamuomba Allâh atuongoze sote katika yenye kumridhisha Yeye. Twamuomba atupe sisi, wewe na Waislamu wote ufahamu na msimamo kwenye Dini.

Sheikh Ibn Baaz

MATONE YA DAMU BAADA YA KUTEKELEZA GHUSL:

SUALI: Nimegundua yakwamba mara nyengine baada ya kutekeleza Ghusl kutokana na ada yangu ya mwezi, baada ya kumaliza ada yangu ya kiwango cha muda wa kawaida, siku tano, nilitokwa na kiwango kidogo sana cha vitone vya damu. Na hii hutokea punde tu baada ya kutekeleza Ghusl. Kisha baadae, hakuna chochote kitokacho. Sasa sijui nifanyeje. Nifuate siku zangu tano za kawaida bila ya kujali yatokeayo baada ya hayo na niendelee kuswali na kufunga? Au niizingatie siku hiyo pia kuwa ni sehemu ya ada yangu nisiswali wala nisifunge katika wakati huo? Ukumbuke yakwamba mambo hayo hayanitokei kila mara isipokuwa hutokea katika kila ada mbili, tatu, au kama hivyo. Natumai utanifaidisha kuhusiana na suala hili.

JAWABU: Ikiwa kinachokutoka baada ya kujitwahirisha ni emma manjano au hudhurungi, haifai kuzingatiwa (kuwa ni heidh) na hukmu yake ni sawa na hukmu ya mikojo.

Hatahivyo, ikiwa inaonyesha wazi kuwa ni damu, itazingatiwa kuwa ni katika sehemu ya heidh na utalazimika kurudia tena Ghusl kutokana na yaliyothubutu kutoka kwa Umm 'Atiyyah (رضي الله عنهما). Mmojawapo wa Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلّم), aliyesema baada ya kutwahirika kutokana na heidh: "Hatukuzingatia chepechepe ya manjano na hudhurungi kuwa na umuhimu wowote."

Sheikh Ibn Baaz

IKIWA MWANAMKE AMEMALIZA ADA YAKE KABLA YA KUTWA KWA JUA, ATALAZIMIKA KUSWALI DHUHR NA 'ASR?

SUALI: Mwanamke mwenye heidh akitwahirika kabla ya kuchomoza kwa jua, atawajibika kuswali Maghrib na 'Ishaa'? Vilevile, iwapo atatwahirika kabla ya kutwa, atawajibika kuswali Dhuhr na 'Asr?

JAWABU: Ikiwa mwanamke mwenye heidh au mwenye damu ya mazazi akitwahirika kabla ya kutwa kwa jua, atalazimika kuswali swala za Dhuhr na 'Asr kulingana na rai yenye nguvu zaidi miongoni mwa wanavyuoni. Vilevile, hiyo ndiyo hali itakavyokuwa akitwahirika kabla ya Alfajiri. Katika hali hiyo, atalazimika kuswali Maghrib na 'Ishaa'. Hii imepokewa na 'Abdur-Rahmaan Ibn 'Auf na 'Abdullaah Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما). Hii ndiyo rai ya Wanavyuoni wengi. Vilevile ikiwa mwanamke mwenye heidh au mwenye damu ya mazazi akitwahirika kabla ya kuchomoza kwa jua, atawajibika kuswali Fajr. Na uwongofu ni kutoka kwa Allâh.

Sheikh Ibn Baaz

MWANAMKE MWENYE HEIDH KUJISAFISHA KUTOKAMANA NA MIKOJO:

SUALI: Ninapokuwa kwenye Heidh, sijisafishi kwa maji kutokamana na mikojo kwa sababu nahofia yakwamba huwenda maji yakanidhuru. Ni nini hukmu kuhusu jambo hilo?

JAWABU: Inatosheleza, badala ya maji kujisafisha kwa karatasi ya shashi (tissue paper) au kitu chochote kigumu kilicho safi kiwezacho kuondoa uchafu ulioko kama vile jiwe, kipande cha mbao au kidutu mfano wake. Kujisafisha huku kutekelezwe kwa mara tatu au zaidi, mpaka uchafu huwo uondoke. Hukmu hii si yako peke yako wala yoyote aliye katika hali kama yako. Hatahivyo, ni kwa Waislamu wote wanaume na wanawake. Hii imetegemezwa juu ya yale yaliyothubutu kutoka kwa 'Aaisha (رضي الله عنهما) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema:
"Anapokwenda mmoja wenu kukidhi haja, na ajisafishe kwa mawe matatu na hiyo itamtosheleza."
Hadeeth hii imepokewa na Ahmad, an-Nasaa'ee na Abu Daawud, na pia Daaraqutnee' aliyesema kuwa silsila yake ya upokezi ni Swaheeh Hasan. Vilevile, imepokewa na Salmaan al-Faarisee (رضي الله عنــه) yakwamba aliambiwa, "Mtume wenu anawafundisha kila kitu, hata jinsi ya kuingia chooni." Akasema Salmaan, "Naam! Ametukataza kuelekea Qibla tukiwa twakidhi haja kubwa au ndogo, tunapojisafisha tupu zetu tusitumie mkono wa kulia, tusijisafishe kwa idadi ya mawe isiyozidi mawe matatu na tusijisafishe kwa kutumia choo kikavu cha Ngamia au mfupa." Hii imepokewa na Muslim, Abu Daawud na at-Tirmidhee.

Sheikh Ibn Baaz

APATA ADA YAKE HALIYAKUWA YUKO MSIKITINI:

SUALI: Mwanamke alijikuta damu inamtoka alipokuwa ndani ya msikiti wa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Alikaa hapo msikitini kwa muda mchache mpaka mumewe alipomaliza kuswali, kisha akaondoka nae. Jee, alichofanya ni madhambi

JAWABU: Iwapo alishindwa kuondoka msikitini peke yake, basi hapana madhara katika aliyoyafanya. Hatahivyo, ikiwa alikuwa na uwezo wa kuondoka peke yake, ni wajibu aondoke haraka iwezekanavyo. Hii ni kwa sababu mwanamke mwenye heidh, mwenye damu ya mazazi na mtu mwenye janaba hawaruhusiwi kukaa msikitini. Hii imetegemezwa juu ya maneno Yake Allâh (سبحانه وتعالى): "Wala wanapokuwa na janaba isipokuwa wanaposafiri barabarani."
Pia imepokewa kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakwamba alisema: "Simruhusu mwanamke mwenye heidh au mtu mwenye Janaba kuingia msikitini."

Sheikh Ibn Baaz

MWANAMKE MWENYE HEIDH ANAWEZA KUSOMA VITABU VYENYE TAFSIRI YA QUR'AN?

SUALI: Nilisoma baadhi ya vitabu vya Tafsiri (Tafsiri ya Qur'an) nikiwa sikutwahirika, kama vile katika wakati wa ada yangu ya mwezi. Jee, kuna madhara yoyote katika jambo hilo? Nimepata madhambi kwa kufanya hivyo? Tafadhali naomba unipe hukmu, Allâh akujazi khari.

JAWABU: Hapana madhara yoyote iwapo mwanamke mwenye heidh au mwenye damu ya mazazi atasoma vitabu vya tafsiri wala katika kusoma kwake Qur'an pasi na kuugusa Mswahafu wenyewe kulingana na rai iliyo na nguvu zaidi miongoni mwa wanavyuoni. Amma kuhusu mtu mwenye Janaba, hafai kuisoma Qur'an kivyovyote mpaka atekeleze Ghusl. Hatahivyo, anaweza kusoma vitabu vya tafsiri, hadeeth na mfano wake bila ya kusoma yaliyomo ndani yake ya aya za Qur'an. Hii imetegemezwa juu ya hadeeth isemayo yakwamba hakuna kilichomuepusha Mtume (صلى الله عليه وسلم) na kuisoma Qur'an isipokuwa akiwa na Janaba. Katika matamshi mengine ya hadeeth, amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم) kama ilivyopokewa na Imaam Ahmad kwa isnad nzuri: "Amma kwa mwenye Janaba, hafai (kusoma), hata aya moja."

Sheikh Ibn Baaz

YARUHUSIWA KWA MWANAMKE MWENYE HEIDH KUSOMA QUR'AN NA VITABU VYA DU'AA'?

SUALI: Inaruhusiwa kwa mwanamke mwenye heidh kusoma kitabu cha du'aa' katika siku ya 'Arafah, tukielewa yakwamba kitabu chenyewe kinaaya za Qur'an?

JAWABU: Hapana madhara kwa mwanamke mwenye heidh au mwenye damu ya mazazi kusoma vitabu vya du'aa' vilivyoandikwa kuhusiana na nguzo za Hajj. Kwa hakika, hapana makosa katika kuisoma kwake Qur'an kulingana na rai iliyo sawa. Hakuna nass iliyo wazi na swaheeh yenye kumkataza mwanamke mwenye heidh au mwenye damu ya mazazi kusoma Qur'an. Kilichopokewa kinahusiana na mtu mwenye Janaba peke yake, yakwamba huyo hafai kusoma Qur'an akiwa kwenye Janaba. Ushahidi huwo umetokana na hadeeth ya 'Ali (رضي الله عنــه) Amma kuhusu mwanamke mwenye heidh au mwenye damu ya mazazi, kuna hadeeth ya Ibn 'Umar (رضي الله عنهما) isemayo: "haifai kwa mwanamke mwenye heidh au mtu mwenye Janaba kusoma chochote kutoka katika Qur'an."
Hatahivyo, Hadeeth hii ni dha'eef. Kwa sababu imepokewa kutoka katika riwaya za Isma'eel Ibn 'Ayyaash kutoka kwa watu wa Hijaaz nae ni dhaifu anapopokea kutoka kwao. Hatahivyo, anaweza kusoma kwa moyo pasi na kuigusa Qur'an. Amma kuhusu mtu mwenye janaba, mke/mume haruhusiwi kusoma hata kwa moyo au kuugusa mswahafu wenyewe mpaka (mke/mume) atekeleze Ghusl. tafauti baina ya hao wawili ni kwamba muda wa wakati wa mwenye janaba ni mfupi sana kwa vile anaweza kutekeleza Ghusl kwa haraka baada ya kufanya kitendo na mwendani wake. Muda wa wakati si mrefu kwa vile yeye ndiye aliye na uwezo wa kumiliki muda wake kwani anaweza kutekeleza Ghusl wakati wowote akijisikiya. Hata kama hawezi kupata maji, anaweza kutekeleza tayammum ili aswali au asome Qur'an. Hatahivyo, mwanamke mwenye heidh au mwenye damu ya mazazi hawezi kumiliki muda wake, uwezo wa kumiliki hayo uko juu ya Mkono wa Allâh. Heidh na damu ya mazazi huchukuwa masiku. Kwahivyo, wao wanaruhusiwa kusoma Qur'an ili wasisahau waliyoyahifadhi vilevile wasikose thawabu za kuisoma. Pia wapate kujifunza hukmu za Shari'ah kutoka katika kitabu cha Allâh. Kwahivyo, anaruhusiwa tena sana kusoma vitabu vya du'aa' vyenye mchanganyiko wa Aya na hadeeth. Hii ndiyo rai ya sawa na maoni ya sawa ya wanavyuoni. Twamuomba Allâh Awarehemu juu ya nukta hii.

Sheikh Ibn Baaz

TANGAZO LA DARSA MASJID MAZRUI

Jumatatu, Jumanne, Jumatano, Alkhamisi na Jumamosi. Darsa zote ni baina ya Maghrib na 'Ishaa'. Nyote munaalikwa kuhudhuria.